HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEFU MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA KUKABIDHI UENYEKITI WA SADC KWENYE MKUTANO WA 40 WA WAKUU WA NCHI WA SADC UNAOFANYIKA KWA MTANDAO, TAREHE 17 AGOSTI, 2020

Mheshimiwa Filipe Nyusi, Rais wa Msumbiji na Mwenyekiti ajaye wa SADC;

Mheshimiwa Mfalme Mswati wa III wa Falme ya Eswatini;

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali Wenzangu wa SADC;

Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya SADC;

Wakuu wa Taasisinyingine za Kikanda na Kimataifa mnaoshiriki nasi kwenye Mkutano huu;

Waheshimiwa Mabalozi;

Maafisa Waandamizi na Wajumbe wengine wa Mkutano;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Tangu tulipokutana mara ya mwisho, Jumuiya yetu imepoteza viongozi kadhaa, ambao ama walikuwa miongoni mwa waanzilishi wa Jumuiya hii, au walishiriki kwenye uanzishaji na pia kutoa mchango mkubwa kwenye Jumuiya yetu. Miongoni mwa viongozi hao ni Hayati Mzee Robert Mugabe, Baba wa Taifa la Zimbabwe; Hayati Mzee Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Hayati Mario Machungo, Waziri Mkuu mstaafu wa Msumbiji. Hivyo basi, kabla ya kuanza hotuba yangu,

naomba angalau tusimame kwa dakika moja, tuwakumbuke. Mwenyezi Mungu azipumzishe Roho zao mahali pema peponi. **Amina.**

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi wenzangu, najisikia furaha na heshima kubwa, leo ninapokabidhi Uenyekiti wa Jumuiya yetu, kuhutubia Mkutano huu ambao unafanyika miaka 40 tangu kuanzishwa kwa Jumuiya yetu mwaka 1980. Lakini, kama mnavyofahamu, Mkutano huu unafanyika katika mazingira ya tofauti sana ukilinganisha na Mikutano mingine ya Wakuu wa Nchi iliyowahi kufanyika kwenye historia ya Jumuiya yetu. Mtakumbuka kuwa, leo hii tulipaswa tuwe tunakutana kwenye Jiji zuri la Maputo nchini Msumbiji kwa ajili ya Mkutano huu, ambako nina uhakika Mheshimiwa Rais Nyusi alikuwa amejipanga kutupokea vizuri. Hata hivyo, kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa *corona (COVID – 19)*, tumeshindwa kukutana ana kwa ana; na badala yake tumelazimika kufanya Mkutano huu kwa njia ya mtandao.

Nitumie fursa hii, kwanza kabisa, kutoa salamu za pole kwa wananchi wote wa Jumuiya yetu walioathirika na ugonjwa huu. Aidha, napenda nizipongeze Nchi zote Wanachama pamoja na Sekretarieti kwa hatua mbalimbali ilizochukua za kukabiliana na ugonjwa wa *corona*. Kama itakavyokumbukwa, kabla ya Shirika la Afya Duniani (*World Health Organization* - WHO) kutangaza ugonjwa wa *Corona* kuwa Janga la Kimataifa; tarehe 9 Machi, 2020, Tanzania, ikiwa Mwenyekiti wa SADC, iliitisha Mkutano wa Dharura wa Mawaziri wa Afya wa SADC kujadili namna ya kukabiliana na ugonjwa huo. Katika Mkutano huo,

miongozo na mikakati mbalimbali ilitolewa kuhusu namna ya kukabiliana ugonjwa huo. Na kutokana na miongozo hiyo, nafarijika kusema kwamba, kwa kiasi kikubwa, tumeweza kuudhibiti ugonjwa huu kwenye Ukanda wetu.

Ni kweli kwamba, zipo athari nyingi ambazo tumezipata kutokana na ugonjwa huu, lakini tumejitahidi sana kulikabili janga hili, tofauti na baadhi ya watu walivyotabiri. Na binafsi naamini, kutokana na mipango na mikakati tuliyonayo, muda sio mrefu tutaweza kuudhibiti kabisa ugonjwa huu, na hatimaye kuweza kurejea tena katika maisha yetu ya kawaida. Jambo la msingi; tuendelee kushirikiana na pia kubadilishana uzoefu wa namna ya kukabiliana na ugonjwa huu. Aidha, hatuna budi kuendelea kuimarisha mifumo yetu ya kutolea huduma za afya napia mikakati ya kukabiliana na majanga. Na katika hilo, nitumie fursa hii kutoa wito kwa Sekretarieti na Nchi Wanachama kushirikiana ili kuharakisha uanzishaji wa Mfuko na Mkakati wetu wa Maafa (*Disaster Risk Preparedness and Response Strategy Fund*). Zaidi ya hapo nitumie fursa hii kurudia rai yangu kwa nchi zilizoendelea kuangalia uwezekano wa kusamehe madeni au kutoa misaada ama mikopo isiyo na riba au yenye masharti nafuu kwa nchi zinazoendelea ili ziweze kukabiliana na athari za kiafya na kiuchumi za ugonjwa wa *corona.*

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Tarehe 17 Agosti mwaka jana, Tanzania ilipata heshima ya kupewa jukumu la kuongoza Jumuiya yetu kwa kipindi cha mwaka mmoja. Leo, tarehe 17 Agosti 2020, tumelikamilisha jukumu hilo na tutalikabidhi kwa wenzetu wa Msumbiji. *Waheshimiwa viongozi*, bila shaka mtakubaliana namimi kuwa, ni matamanio ya kila mtu kwamba, unapopewa jukumu la kuongoza Taasisi yoyote, siku unapolikamilisha, uwe umetoa mchango ambao utakuwa umesaidia kuisogeza mbele Taasisi au Jumuiya hiyo, kuliko ulivyoikuta.

Ni kwa msingi huo, leo ninapokabidhi jukumu hili la Uenyekiti kwa ndugu na marafiki zetu wa Msumbiji, sisi Watanzani tunafarijika sana kuona kuwa, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, tumeweza kutoa mchango wetu, ambao bila shaka, utakuwa umesaidia kuisogeza mbele Jumuiya yetu. Kwa hakika; kutokana na ushirikiano mkubwa tulioupata kutoka kwa Nchi zote Wanachama pamoja na Sekretarieti, tumeweza kupata mafanikio makubwa karibu kwenye maeneo yote: kuanzia kwenye masuala ya siasa, ulinzi na usalama; utawala bora na demokrasia; utengamano wa kiuchumi, masuala ya kijamii, n.k. Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Kama nyote mjuavyo, moja ya maeneo muhimu ya kipaumbele kwa Jumuiya yetu ni ulinzi na usalama. Nafarijika kutamka kuwa, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, tumejitahidi kusimamia jukumu hilo kikamilifu, hususan kwa kuhakikisha amani na usalama

unaendelea kutawala kwenye Ukanda wetu na pia kushughulikia baadhi ya migogoro iliyopo, ikiwemo nchini DRC na Lesotho. Nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama (*SADC Organ*), kaka yangu, Mheshimiwa Rais Mnangagwa wa Zimbabwe, kwa jitihada zake za kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Nawapongeza pia wananchi wa Lesotho kwa kufikia makubaliano ya Amani chini ya Usuluhishi wa Jamhuri ya Afrika Kusini, ambayo yamepelekea kuteuliwa kwa Mheshimiwa Moeketsi Majoro, kuwa Waziri Mkuu wa Nchi hiyo baada ya kustaafu kwa Mheshimiwa Thomas Thabane. Ni imani yangu kuwa hatua hii itaimarisha amani na utulivu nchini Lesotho na kuwawezesha raia wa nchi hiyo kujikita kwenye shughuli za maendeleo.

Na katika hilo, nitumie fursa hii pia kumkaribisha rasmi Mheshimiwa Majoro kwenye Jumuiya yetu. Aidha, nawapongeza na kuwakaribisha Waheshimiwa Marais Prithvirajsing Roopum wa Mauritius na Dkt. Lazarus Chakwera wa Jamhuri ya Malawi, ambao wamechaguliwa hivi karibuni. Vilevile, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Marais Dkt. Mokgeetsi Eric Keabetswe Masisi wa Botswana; Mheshimiwa Filipe Nyusi wa Msumbiji; Dkt. Hage Geingob wa Namibia, ambao wamechaguliwa tena kuongoza mataifa yao. Uchaguzi wa viongozi hao ni ishara ya kukomaa kwa misingi ya demokrasia katika Jumuiya yetu.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Mbali na masuala ya amani, ulinzi, usalama pamoja na utawala bora, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, tumejitahidi pia kusimamia masuala ya utengamano wa kiuchumi. Itakumbukwa kuwa, wakati wa Mkutano wa 39 Wakuu wa Nchi tulizindua Mfumo wa Uombaji na Utoaji Vyeti vya Utambuzi wa Uasili wa Bidhaa kwa njia ya mtandao (*e-certificate on rules of Origin*). Kuzinduliwa kwa mfumo huu kutarahisisha ufanyaji biashara mipakani hususan kwa wafanyabiashara wetu wadogo. Itakumbukwa pia kuwa, mwaka jana, wakati Tanzania ikiwa mwenyeji wa Maadhimisho ya Maonesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya SADC lilizinduliwa Baraza la Biashara la SADC (*SADC Business Council*). Ni wazi kuwa kuanzishwa kwa Baraza hili, kutachochea shughuli za uzalishaji na kuimarisha ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, ambayo ni muhimu katika kujenga uchumi wa kisasa.

Vilevile, kutokana na kuibuka kwa ugonjwa wa *corona,* SADC chini ya Uenyekiti wa Tanzania ilisimamia uandaaji wa Miongozo kwa ajili ya Kuoanisha Taratibu za kufanya Biashara kwenye maeneo ya Mipakani (yaani *Regional Guidelines on Harmonization and Facilitation of Cross Border Transport of Goods*). Hii imewezesha wanachi wetu kuendelea kufanya biashara licha cha kuwepo kwa ugonjwa wa *corona;* na hivyo, kupunguza athari za kiuchumi kwa wananchi lakini pia, nchi zetu kwa ujumla. Sambamba na hayo, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, tumeendelea kusimamia ajenda muhimu ya Jumuiya

kwa sasa kuhusu maendeleo ya viwanda. Kwa kutumia kaulimbiu ya Mkutano wa 39, isemayo *"Mazingira Wezeshi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya Viwanda, Biashara na Ajira ndani ya SADC"*, tulijitahidi kuzihimiza Nchi Wanachama kuweka kipaumbele sio tu katika kujenga vipanda lakini pia kutengeza mazingira mazuri ya kustawisha ukuaji wa sekta ya viwanda kwenye Ukanda wetu. Na kama nyote mnavyofahamu, moja ya kichocheo muhimu cha kustawisha sekta ya viwanda, ni upatikanaji wa umeme wa uhakika. Ninayo furaha kuuarifu Mkutano huu kuwa, katika kipindi mwaka mmoja uliopita, Jumuiya yetu imeongeza **megawati 3,595** za umeme; sawa na **asilimia 90** ya lengo la kuzalisha **megawati 4000**. Aidha, baadhi ya nchi zimesaini Makubaliano ya kutekeleza Miradi ya Pamoja ya Kusafirisha Umeme (*Inter-Governmental Memorandum of Agreements*-IGMoA) kupitia programu ya *Southern African Power Pool* (SAPP). Makubaliano yaliyosainiwa nikati ya Tanzania na Zambia na kati ya Malawi na Msumbiji.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Katika mwaka mmoja uliopita pia tumeweza kusimamia uandaaji wa Ajenda za Maendeleo za SADC baada ya Mwaka 2020. Kama mnavyofahamu, tangu mwaka 2000, ajenda za maendeleo za Jumuiya yetu zimekuwa zikisimamiwa na mikakati mikuu miwili: Mpango Mkakati Elekezi wa Maendeleo ya Kikanda (yaani *Regional Indicative Strategic Development Plan - RISDP*) wa mwaka 2015 na Mpango Mkakati wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama Awamu ya Pili (yaani *Strategic*

Indicative Plan for the Organ - SIPO II). Mikakati hii yote inafikia ukomo mwishoni mwa mwaka huu (2020). Hivyo basi, katika kipindi cha Uenyekiti wetu, tumeweza kuandaa Dira ya Maendeleo ya SADC 2050 pamoja na Mpango Elekezi wa Maendeleo ya Kikanda (RISDP) wa mwaka 2020 - 2030. Ni imani yangu kuwa, nyaraka hizi mbili ambazo zitajadiliwa kwenye Mkutano huu, zitatoa mwelekeo mpya wa kufikia malengo yetu ya *"SADC Tunayoitaka".*

Mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha Uenyekiti wetu ni kuridhiwa kwa lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha nne za SADC, ambayo kwa kuanzia inatumika kwenye vikao vya ngazi ya Wakuu wa Nchi. Ni imani yangu kuwa kuridhiwa kwa lugha hii kwanza ya Kiafrika kwenye Jumuiya yetu, kutachochea ushirikiano na utengamano ndani ya Jumuiya. *Na hii ndiyo sababu nimeamua kutoa hotuba yangu kwa Kiswahili na nimefarijika kuwaona kuwa, wengi wenu, mnanisikiliza bila kutumia vifaa vya kutafsiri. Hii inaonesha kuwa mnaifahamu na kuielewa vyema lugha hii adhimu ya Kiswahili.*

Ukiachilia mbali hilo, itakumbukwa kuwa, kwenye Mkutano wa 39, tulipitisha Azimio la kuondolewa vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa dhidi ya Jamhuri ya Zimbabwe tangu mwaka 2000. Kwenye Azimio hilo pia tuliipitisha tarehe 25 Oktoba ya kila mwaka kuwa ni Siku Maalum ya Kupinga Vikwazo ilivyowekewa Zimbabwe, ambapo Nchi Wanachama zitakuwa zikiadhimisha kwa kufanya mambo mbalimbali, ikiwemo kuandaa makongamano, midahalo au

kutoa matamko yenye kupinga vikwazo kwa Zimbabwe. Inatia moyo kuona kuwa, kama tulivyokubaliana, tarehe 25 Oktoba 2019 tulitekeleza Azimio hilo. Vilevile, baadhi yetu, tulijumuisha suala la kuondolewa kwa vikwazo kwa nchi ya Zimbabwe kwenye Hotuba zetu kwenye Mkutano wa 74 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, lakini pia kwenye majukwaa mbalimbali ya kimataifa.

Kutokana na hatua hizo, baadhi ya mafanikio yameanza kupatikana. Mathalan, Umoja wa Ulaya (EU) umeanza kuona umuhimu wa kutatua mgogoro wa kibinadamu nchini humo kwa kutoa misaada na kuonesha utayari wa kusaidia utaalamu kwenye sekta mtambuka za maendeleo ya uchumi, huduma za msingi za afya, kuijengea uwezo Zimbabwe kuhimili maafa na kufanikisha utoaji wa misaada mingine ya kibinadamu. Sambamba na hilo, Benki ya *"The Herald Agribank"*pamoja na Benki ya *"Infrastructure Development Bank"* nchini Zimbabwe zimeondolewa kwenye orodha ya vikwazo vilivyowekwa na EU. Nazishukuru nchi na taasisi zoteza kimataifa zilizoanza kuitikia wito wetu wa kuiondolea vikwazo nchi ya Zimbabwe, ambavyo vimekuwa na athari kubwa kwa wananchi wa Zimbabwe, hususan wanawake, wazee na watoto. Nina imani, mataifa mengine yataiga mfano ulioanza kuoneshwa na Umoja wa Ulaya. Zimbabwe ikiondolewa vikwazo, itatoa mchango mkubwa sio tu kwenye Jumuiya yetu bali duniani kwa ujumla.

Waheshimiwa Viongozi, kwa kifupi sana, haya ni baadhi tu ya mafanikio yaliyopatikana kwenye kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Nitumie fursa hii kuzishukuru tena Nchi zote Wanachama kwa ushirikiano mkubwa mliotupatia. Bila ushirikiano wenu, mafanikio yote niliyoyataja, kamwe yasingepatikana. Kwa namna ya pekee sana, naishukuru Sekretarieti chini ya uongozi wa mwanamama mahiri, jasiri na shupuvu, Dkt. Stergomena Lawrence-Tax, kwa kufanya kazi kwa kujituma na ueledi mkubwa, licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali, ikiwemo ugonjwa wa *corona* pamoja na majanga ya vimbunga na mafuriko yaliyoikumba Jumuiya yetu. Hivyo basi, naishukuru sana Timu yote ya Sekretarieti kwa ushirikiano walionipatia. Napenda pia niwashukuru Washiriki wa Maendeleo kwa kutuunga mkono katika jitihada zetu za kufikia malengo endelevu katika Ukanda wetu.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu; na kama nilivyogusia mwanzoni, mwaka huu Jumuiya yetu imetimiza miaka 40 tangu ilipoanzishwa mwaka 1980. Katika kipindi hicho, mafanikio mengi makubwa yamepatikana. Idadi ya nchi wanachama imeongezeka kutoka **9** waanzilishi hadi kufikia **16** hivi sasa; idadi ya watu nayo imeongezeka kutoka takriban **milioni 60** hadi kufikia takriban **milioni 350** hivi sasa. Miundombinu imeimarika, biashara miongoni mwa Nchi Wanachama imeongezeka kutoka **asilimia 5** hadi kufikia takriban **asilimia 20** hivi sasa; hali ya maisha na vipato cha wananchi wetu

kimekua; na amani na usalama imetawala kwenye Ukanda wetu kuliko eneo jingine lolote Barani Afrika.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, bado tuna safari ndefu ya kuweza kutimiza ndoto na dhamira ya waasisi wa Jumuiya hii. Kama nilivyosema wakati nikipokea Uenyekiti, wananchi wetu wengi bado ni masikini, na wanakabiliwa na matatizo ya njaa, magonjwa na ukosefu wa ajira licha kwamba eneo letu limebarikiwa kuwa rasilimali nyingi, ikiwemo ardhi yenye rutuba, madini, misitu, mifugo, rasilimali za maji, n.k. Aidha, hata kiwango chetu cha biashara bado kipo chini ukilinganisha na maeneo mengine, ambapo nchi za Amerika Kusini wastani wake ni **asilimia 40,** Asia hivi sasa ni**asilimia 60** na Ulaya ni **asilimia 60**. Eneo letu pia bado linakabiliwa na changamoto za migogoro.

Changamoto hizo pamoja na nyingine zilizoibuka hivi karibuni, ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, matishio ya ugaidi, uhalifu wa kimataifa na sasa ugonjwa wa *corona*, zinatukumbusha kuhusu umuhimu wa kuendelea kushirikiana na kushikamana. Na binafsi naamini, endapo tutashirikiana na kufanya karibu, Jumuiya yetu inao uwezo mkubwa wa kuzishinda changamoto hizo, kama tulivyozishinda changamoto nyingine zilizowahi kuibili Jumuiya yetu, ikiwemo utumwa; ukoloni na bila kusahau ubaguzi wa rangi.

Waheshimiwa Viongozi, baada ya kusema hayo, sasa ninayo furaha kukabidhi Uenyekiti wa Jumuiya yetu kwa ndugu yangu, ambaye pia ni rafiki mkubwa wa Tanzania, Mheshimiwa Filipe Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji. Nina matumaini makubwa, chini ya uongozi wake, kutokana na uzoefu alionao yeye binafsi pamoja na nchi yake, atatoa mchango mkubwa katika kushughulikia baadhi ya changamoto nilizozitaja, na hasa kwa kuzingatia ule usemi wa wahenga usemao, "*Maisha huanza baada ya miaka 40*". Hivyo basi, kwa kuwa Jumuiya yetu imetimiza miaka 40, nina uhakika sasa tutaanza kuona maendeleo kwa kasi zaidi. Kwa upande wetu sisi Tanzania, kama ilivyoada, tunaahidi kumpa Mwenyekiti mpya, ushirikiano wa kutosha.

Mungu Ibariki SADC!

Mungu Ibariki Afrika!

"Thank you very Much"

"Merci beaucoup"

"Muito Obrigado"

"Ahsanteni sana kwa Kunisikiliza"